# Zaburi 32

SIKU YA MUNGU YA TANO YA PASKA/ Mwaka A

*Gauthier KM*




1. Mshangilieni Bwana, enyi wanyofu,
kumsifu kunawafaa waamini .
Mtukuzeni Bwana kwa kinubi ,
mpigieni kinanda cha nyuzi kumi .

2. Maana neno la Bwana ni lakweli ,
matendo yake yote ni maaminifu.
Apenda unyofunahaki ,
dunia imejaa wema wake Bwana.

3. Macho ya Bwana yawaelekea wanao mheshimu,
wale wanaotumainia wema wake.
Ili aopoe roho yao katika kifo,
na wakati wa njaa awalishe.